MATUNDASI ASM DEVELOPMENT COMPANY LIMITED

https://www.matundasiasm.co.tz/ info@matundasiasm.co.tz

**28 Mei, 2025**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Matundasi ASM Development Company Limited (MADC) ni kampuni inayojishughulisha na utafiti na uchimbaji wa madini katika Mkoa wa Mbeya, wilaya ya Chunya. Kampuni hii inawatangazia wote wenye sifa tajwa kuwasilisha maombi ya kuajiriwa katika nafasi mbalimbali kama ifuatavyo:

**OPERETA MITAMBO MIKUBWA YA UJENZI (Heavy Duty Earth Moving Equipments)**

**OPERETA MITAMBO MIKUBWA YA UJENZI DARAJA LA III (HEAVY DUTY EARTH MOVING EQUIPMENT) - Nafasi mbili (02)**

**SIFA ZA MUOMBAJI:**

- Trade Test Daraja la III (au cheti kinachoendana) katika kuendesha mitambo mikubwa.
- Uwezo wa kutumia vifaa vizito kama vile Bulldozer, Excavator, Tractor, Grader, Malori Makubwa ya Migodini (Mining Dump Trucks) na vinginevyo.
- Uwezo wa kutumia vifaa katika mazingira mbalimbali.
- Uelewa wa masuala ya afya na usalama kazini (HSE)
- Uwezo wa Kuandika kumbukumbu na ripoti za kila siku ili kufuatilia matumizi na matengenezo ya kifaa
- Uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi, uchimbaji madini, au tasnia zingine zinazohusiana,
- Muombaji awe na umri usiozidi miaka 30

**NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:**

- Maombi yaelekezwe kwa:
  **Afisa Rasilimali Watu**
  Matundasi ASM Development Company Limited,
  S.L.P 70812,
  DAR ES SALAAM,
- Maombi yote yatumwe kupitia barua pepe info@matundasiasm.co.tz na hr@matundasiasm.co.tz
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **20 Juni, 2025,** na kichwa cha barua pepe kiwe jina la nafasi unayoomba.

**VIAMBATANISHO MUHIMU**

- Waombaji wenye sifa wanatakiwa kuwasilisha barua ya maombi ikiwa na nyaraka zifuatazo:
    a) Nakala za vyeti husika (vilivyothibitishwa),
    b) Nakala ya leseni
    c) Nakala ya cheti Cha utumishi (kampuni aliyotoka)
    d) Picha mbili (2) za pasipoti za hivi karibuni,
    e) Wasifu binafsi (CV)
    f) Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA)
    g) Police Fingerprint.
    h) Wadhamini watatu (wa nje na ndani ya familia ikiwa na picha za wadhamini na anuani zao (nambari za simu)
    i) Barua ya wadhamini watatu, mmoja (01) wa nje na wawili (02) wa familia pamoja na picha(passport) zao na mawasiliano yao yanayopatikana.
    j) Barua ya utambulisho kutoka serikali za mtaa anapotokea.
- Waombaji waliotimiza vigezo ndio watakaoitwa kwa ajili ya usaili.

MATUNDASI ASM COMPANY LTD